

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI



NIULIZE KUHUSU FURSA ZA UWEKEZAJI MANISPAA YA LINDI

0718 340 247


0713 548 374

0767 042 958

Barua Pepe: info@lindimc.go.tz

- Baada ya kuongezewa jimbo la Mchinga, kwasasa Manispaa ya Lindi inadhaniwa kuwa ndio Manispaa yene eneo kubwa zaidi la utawala kuliko Manispaa zote nchini kwani inakadiriwa kuwa na eneo lenye ukubwa wa kilometra za mraba zaidi ya 3900. Kwa mijibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, majimbo yote mawili yalikuwa na jumla ya wakazi takribani 142,142 na hivyo kuwa mionganoni mwa Halmashauri zenyi idadi ndogo zaidi ya wakazi. Hapa chini ni mlinganisho wa Manispaa ya Lindi na baadhi ya Halmashauri ya Manispaa nyiningine kwa ukubwa wa eneo na idadi ya wakazi.

JINA LA MANISPAA	UKUBWA WA ENEO (KILOMETRA ZA MRABA)	IDADI YA WATU (SENSA 2012)
Moshi	58	184,292
Mtwara	163	108,296
Songea	616	131,336
Kinondoni	321	926,681
Morogoro	360	315,866
Lindi	3900	142,142



Muonekana wa Manispaa ya Lindi kwa majimbo

- Ndipo unajengwa mtambo mkubwa wa kisasa wa uchakataji Gesi Asilia (LNG plant) wenyewe thamani ya USD 30Billion sawa na Tshs 70 Trillioni . mradi huu unatarajiwa kuwa wenyewe thamani zaidi kuwahi kutokea kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati. Utakuwa na uwezo wa kulisha viwanda vingine vingi vitakavyokuwa vikitumia **by products** zake. Jirani na eneo hili la LNG limetengwa eneo lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 15,000 kwa ajili ya viwanda hivyo tarajiwa (Petro Chemical Industries). Kupitia uwekezaji huo, ajira nyingi zinatarajiwa kuzalishwa nchini.



- Ndio Manispaa inayojishughulisha na kilimo na ufugaji kwa kiwango kikubwa kuliko Manispaa zote nchini, hii inatokana na kuwa na eneo kubwa lenye Uoto mzuri na vyanzo vyta kutosha vya Maji. Mwaka 2017/18 zaidi ya ekari 40,000 ziligawiwa kwa watu /taasisi mbalimbali kwa ajili ya Uwekezaji wa Kilimo cha Korosho na Ufuta. Mazao haya kwasasa ndiyo yanaongoza kwa kuliingizia Taifa fedha za Kigeni. Maeneo bado yanaendelea kutolewa kwa watu na taasisi zenye mahitaji ya uwekezaji.




Korosho ambayo haijabanguliwa



Korosho iliyobanguliwa



Ufuta ukiwa umeanikwa baada ya kuvunwa



Ufuta ukiwa tayari kwa ajili ya matumizi

- Pia ina eneo la fukwe lenye urefu wa zaidi ya kilometra 200 zinazosadikiwa kuwa mionganini mwa fukwe nzuri na bora kabisa duniani. Maeneo haya ambayo hayajatumika kikamilifu yanafaa kwa ajili ya shughuli za Kitalii, mapumziko, michezo na uvuvi. Kutokana na uwekezaji mkubwa wa kiwanda cha kuchakata Gesi Asilia (LNG) , ni dhahiri kuwa mahitaji ya huduma za hoteli na maeneo ya burudani fukweni yatakuwa makubwa. Tunakaribisha maombi ya uwekezaji katika eneo hili.



Fukwe za bahari mkoani Lindi - Wilaya Lindi Mjini



- Mjusi mkubwa kabisa kuwahi kutokea duniani “dynasol”, aliyehifadhiwa kwenye makubusho yenyе hadhi kubwa duniani yaliyopo Ujerumanı aligunduliwa eneo la Kitendaguru lilipo Manispaa ya Lindi. Kuna vivutio vingi vya Utalii ambavyo vimeweza kuivutia kampuni kubwa ya Utalii duniani ya **Grumeti** kufikiria kuja kuwekeza (mazungumzo yanaendelea), karibu uwe sehemu ya maendeleo ya Uchumi wa nchi yetu.



- Halmashauri ina maeneo mengi yenye akiba kubwa sana ya madini ya "Gypsum" na "graphite". Uwepo wa madini haya muhimu kwa matumizi ya viwandani, yanathibitisha kuwa Lindi ndio sehemu sahihi ya uwekezaji kwa taasisi na mwanachi mmoja mmoja.




Madini ya Gypsum




Madini ya Graphite

- Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo cha Taifa cha Usafirshaji (NIT) ni miongoni mwa taasisi zilizoweza kubaini "potentials" zilizopo Manispaa ya Lindi na sasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kipo hatua nzuri ya uanzishaji wa Ndaki ya Kilimo na Teknolojia ya Uvumi (College of Agriculture and Fisheries Technology) eneo la Ngongo, aidha Chuo cha Taifa cha Usafirshaji nao wapo hatua nzuri wa Uanzishaji wa Ndaki ya Usafirshaji Majini na masuala ya Mafuta (Maritime studies and Petroleum Technology eneo la Kikwetu)



The College of Agriculture and Fisheries Technology (UDSM) eneo la Ngongo



The College of Maritime studies and Petroleum Technology (NIT) eneo la Kikwetu

- Kwa asiyefahamu, Manispaa ya lindi ndiyo Manispaa ilio karibu zaidi na jiji la Dar_es_salaam, baada ya Manispaa ya Morogoro. Ni kwababu hiyo tunadhani kuna kila sababu ya watu na taasisi mbalimbali kuchangamkia fursa zilizopo ikiwa ni pamoja na kununua viwanja vya KIKWETU na NGONGO.

Viwanja vinauzwa kwa bei rafiki kama ifuatavyo

Na	MATUMIZI YA ARDHI	BEI YA KWA KILA MITA YA MRABA
1	Makazi	2,500/=
2	Makazi na biashara	3,000/=
3	Majengo ya umma (public building) taasisi, zahanati, huduma za ibada (religious institution), taasisi za elimu, shule.	2,500/=
4	Biashara, Hoteli, Taasisi binafsi, Housing Estate	4,500/=